

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI YA KISWAHILI

JUNI / JULAI - 2012

SAA 2 ½

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA WILAYA YA BUTERE- 2012

Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI YA KISWAHILI

JUNI / JULAI - 2012

SAA 2 ½

MAAGIZO

- (a) Jibu maswali **manne** pekee .
- (b) **Swali la kwanza ni la lazima**
- (c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani :*
Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
- (d) **Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.**

*Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

SEHEMU YA A: USHAIRI

Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo
Kwacho, lijalo na lije, nimechoka vumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuuko, maudhui tuyasikiayo
Nayo, visa nazmauko, wanyonge wayakutayo
Kwayo, sima zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanotulimiya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaoumiya, na maafa wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine,kwao liko angamiyo
Hawa, uwapa unene, watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tafauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado , tuling'owe shina, ulaji pia na moyo
Naandika!

Maswali

- a) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari zipi?
Thibitisha kila jibu lako (ala4)
- b) Eleza dhamira ya mshairi (ala2)
- c) Onyesha mifano miwili ya uhuru wa kishairi jinsi ulivyotumika katika shairi (ala2)
- d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (ala4)
- e) Tambulisha kwa mifano mbinu zozote mbili za sanaa katika shairi. (ala2)

- f) fafanua sifa za kiarudhi zilizotumika katika mbeti wa tano. (ala3)
- g) Eleza maana ya maneno haya kama yaliyotumiwa katika shairi. (ala3)
- i) Zuiliko
 - ii) Wavune
 - iii) Wenye pupa na kamiyo.

SEHEMU YA B: RIWAYA

S.A MOHAMMED - UTENGANO

Jibu swali la 2 au 3

2. “Inani yake ni kwamba, mwanamke angaliweza kufanya lolote alifanyalo mwanamme pindi akipewa nafasi”
- a) Eleza muktadha wa dondo hili (ala 4)
 - b) Fafanua sifa sita za mrejelewa katika dondo hili (ala 6)
 - c) Huku ukitoa mifano, thibitisha ukweli wa kauli hii kuwa mwanamke angaliweza kufanya lolote alifanyalo mwanamme kwa mujibu wa riwaya hii (ala 10)
3. “Mwiba wa kujichoma hauna Kilio. Dhibitisha kauli hii ukirejelea Riwaya ya Utengano (ala 20)

SEHEMU YA C: TAMTHILIA KITHAKA WA MBERIA - KIFO KISIMANI

Jibu swali la 4 au 5

4. “ Si vyema kuachilia Butangi kuperomoka. Hatuwezi kuendelea kuahirisha kusuluhisha tatizo hili”
- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (ala 4)
 - b) Ni mapendekezo gani yaliyotolewa wakati wa usemi huo kuhusiana na kulitatua tatizo hili? (ala 6)
 - c) Anayeleta tatizo anaotea Butangi mambo mengi. Yataje. (ala 7)
 - d) Mwenye kusuluhisha tatizo alipewa ahadi. Zitaje (ala 3)

5. Eleza namna mwandishi wa kifo kisimani aliyofanikiwa katika matumizi ya mbinu hizi
- i) Chuku (ala 10)
 - ii) Taharuki (ala 10)

SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI

6. a) Tofautisha kati ya methali na semi. (ala 2)
- b) Toa miwili miwili ya methali zinazozingatia tamathali zifuatazo
- i) Ba1agha (ala 2)
 - ii) Takriri (ala 2)
 - iii) Ukinzano (ala 2)
- c) Fafanua vijipera vifuatavyo vya mazungumzo
- 1. Utani (ala 2)
 - 2. Soga (ala 2)
 - 3. Ulumbi (ala 2)
- ii) Taja sifa na umuhimu wa soga (ala 6)

SEHEMU YA E : HADITHI FUPI

K.W. WAMITIKA - MAYAI WAZIRI WA MARADHI WA HADITHI NYINGINE

7. Kwa kurejelewa hadithi tano za diwani ya mayai waziri wa maradhi na Hadithi Nyingine tetea kauli kuwa, << Maudhui ya haki za watoto yamejadiliwa kinagaubaga. (ala 20)